SHIRIKA LA RELI TANZANIA

# RELI na MATUKIO

Gazeti Kila Mwezi



Julai 13, 2020

Gazeti la Reli | Toleo Namba 8 | Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

# RAIS MAGUFULI AWEKA JIWE LA MSINGI LA UJENZI WA MAHANDAKI YA RELI YA SGR NA KUTEMBELEA MRADI DAR - KILOSA



Na Mwandishi wetu TRC

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt John Pombe Magufuli aweka jiwe la msingi la ujenzi wa mahandaki ya reli ya kisasa - SGR na kutembelea mradi Dar es Salaam hadi Kilosa mkoani Morogoro kuanzia tarehe 28 – 29 Juni 2020.

Katika ziara yake Mhe. Rais aliongozana na Mkuu wa Majeshi Jenerali Venance Mabeyo, Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Isack Kamwelwe, Waziri wa Nishati Mhe. Medard Kalemani, Mkuu wa Jeshi la Polisi Simon Sirro, Mkuu wa mkoa wa Dodoma Mhe. Bilnith Mahenge, Wakuu wa mikoa na wilaya, viongozi wa Dini na Chama cha Mapinduzi – CCM pamoja na uongozi wa Shirika la Reli Tanzania ukiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Prof. John Wajanga Kondoro na Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa.

Mheshimiwa Rais amesema kuwa ameridhishwa na maendeleo ya mradi na amewapongeza wakandarasi kwa kazi nzuri wanayofanya ambapo kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro mradi huo umefika zaidi ya 83% na kipande cha Morogoro – Makutupora mradi umefika zaidi ya 38%

“Wakandarasi mnafanya kazi nzuri, nimeona kazi za ‘Structure’ kule na nina uhakika mpaka kwenda huko mbele wamefanya kazi nzuri, nataka nihakikishe wanamaliza mapema, wananchi wa Soga na wananchi wote watumie usafiri huu kwa sababu ni muhimu katika maisha yao” alisema Mhe. Rais

Rais Magufuli amesema kuwa mradi wa SGR unatumia fedha nyingi ambazo ni mapato ya ndani hivyo kuna haja ya kuhakikisha wananchi wanaoishi katika maeneo ya mradi wananufaika na mradi huo kwa kupata huduma za afya, maji, elimu na fursa za biashara katika maeneo ambayo mradi huo umepita hususani Stesheni mpya zinazojengwa.

>> Inaendelea Uk. 2

Na Mwandishi wetu TRC Inatoka Uk 1



# RAIS MAGUFULI AKAGUA MRADI WA SGR NA KUWEKA JIWE LA MSINGI LA UJENZI WA MAHANDAKI YA RELI



"Mradi huu unagharimu fedha nyingi, ni zaidi ya Trilioni 7 na fedha zote hizi zimetolewa na watanzania, ninataka hapa pawe pazuri, na hawa wananchi wenye uwezo wa kufanya biashara wafanye ili wafaidike na hii treni" alisema Mhe. Magufuli

Rais Magufuli aliongeza kuwa jitihada hizi za utekelezaji wa miradi mikubwa ni za watanzania kwani wameweza kutekeleza mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kwa kutumia fedha zao wenyewe

"Sikutegemea kama siku moja Tanzania tutakuwa na Mahandaki kama haya na Mahandaki yenyewe yajengwe na fedha za watanzania masikini, leo mimi mwenyewe nimekuwa shahidi wa mafanikio haya makubwa yaliyopatikana, ninamshukuru sana Mungu" alisema Rais Magufuli

Mahandaki 4 yenye jumla ya urefu wa Kilometa 2.7 yanajengwa katika Mradi wa SGR kipande cha Morogoro – Makutupora katika eneo la Kilosa ambapo handaki refu zaidi lenye urefu wa Kilometa 1.031 tayari limekamilika sambamba na mahandaki mengine matatu ambayo yote kwa pamoja yataunganishwa na madaraja ili kuepusha athari za mafuriko ya mto mkondoa.

"Ujenzi wa Mahandaki manne ambayo yote kwa pamoja yatakuwa na urefu wa Kilometa 2.7 pamoja na daraja la mita 500 litakalounganisha Mahandaki haya" alisema Mhe. Magufuli

"Wakati ninapanga kujenga reli, watu wengi hawakuamini, ni kipindi ambacho treni ya kwenda Moshi na Arusha ilikuwa imekufa, treni za kwenda Tabora na Kigoma zilikuwa zinasuasua lakini pia ni kipindi ambacho hapa Kilosa njia ya reli ilikuwa inajifunga kutokana na mafuriko, kwa mazingira hayo wapo walioniona ninaota mchana lakini nilimuamini Mungu na watanzania masikini" aliongeza Rais Magufuli

Katika kuhakikisha treni za umeme zinafanya kazi kiufanisi pindi mradi utakapoanza Waziri wa Nishati Mhe. Medard Kalemani amewahakikishia wananchi wa Kilosa na watanzania kwa ujumla kuwa serikali inatekeleza Miradi ya uzalishaji umeme ikiwemo Mradi mkubwa wa Bwawa la Mwl. Nyerere ili umeme uwepo kwa uhakika na kuwezesha treni kutoa huduma kwa ufanisi pindi mradi utakapokamilika.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa amesema kuwa mradi unaendelea vizuri huku watanzania wakiendelea kunufaika na mradi huo kwa kupata kipato na kuongeza pato la taifa kupitia kodi wanazolipa wakandarasi

"Mpaka sasa hivi Wakandarasi kwa maana kuna wengine wanaleta nyama, sukari, maziwa mpaka sasa hivi pesa ambayo imerudi nchini ukiacha kodi ni Dola Milioni 576 hiyo ni pesa ambayo imeenda kwa watanzania wenzetu" alisema Kadogosa

Katika taarifa yake Ndugu Kadogosa ameongeza kuwa "Reli yetu ya zamani imepita kandokando ya mto umbali wa Kilometa 120, hivyo kila mwaka tunatumia fedha nyingi za watanzania kurudishia reli iliyochukuliwa na maji, kwahiyo (ujenzi wa Mahandaki) huu ni muarobaini kwamba hatutakuwa na tatizo na reli yetu ya kisasa katika mto Mkondoa"

Mhe. Rais amewaomba wananchi wote kwa ujumla kuendelea kutoa ushirikiano katika kulinda miundombinu ya reli na mradi huo ili kuhakikisha mradi huo unaisha kwa wakati kwa ajili ya manufaa yao na taifa kwa ujumla. Pia katika kulekea kipindi cha uchaguzi Mheshimiwa Rais Magufuli amewaomba watanzania kuendelea kutunza amani iliyopo ili kuwezesha shughuli za kimaendeleo kufanyika na kusaidia kukuza pato la taifa kwani endapo hakutakuwa na amani nchi haitaweza kutekelea miradi ya kimaendeleo kama huu wa ujenzi wa reli ya kisasa.

# RAIS MAGUFULI ALIPONGEZA SHIRIKA LA RELI TANZANIA, UJENZI WA RELI YA KISASA DAR ES SALAAM - MOROGORO MBIONI KUKAMILIKA



Na Mwandishi wetu TRC

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli amelipongeza Shirika la Reli Tanzania – TRC kwa kusimamia vizuri mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR ambao hivi sasa upo mbioni kukamilika kwa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro chenye urefu wa Kilometa 300 na kipande cha Morogoro - Makutupora chenye urefu wa Kilometa 422 ambao umefikia asilimia 30, katika hotuba aliyoisoma Bungeni jijini Dodoma hivi karibuni, Juni 2020.

Rais Magufuli aliyazungumza hayo wakati wa Hotuba yake ya kufunga Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Juni 16, 2020 ambapo alieleza mafanikio kadhaa ambayo serikali ya awamu ya tano imefanya kwa kipindi cha miaka mitano ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora Singida ambapo ufadhili wa mradi huo ni fedha za ndani kwa asilimia 100.

“Miradi hii miwili inagharimu shilingi trilioni 7.062, na fedha zote zinatolewa na serikali kwa asilimia mia moja” alisema Rais Magufuli

Rais Magufuli alisema kuwa Ujenzi wa sehemu ya Mwanza, Isaka hadi Dodoma upo kwenye mikakati ya kutangazwa hivi karibuni ili ujenzi wa sehemu hizo uanze na kuunganisha vipande hivyo kutokea Dar es Salaam na Mwanza kwa lengo la kukamilisha awamu ya kwanza ya mradi huo kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza kwa haraka zaidi.

Aidha, Rais Magufuli alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitano Serikali imefanikiwa kufufua usafiri wa reli ya kati Dar es Salaam, Tanga, Moshi hadi Arusha ambao safari za treni zilisimama takribani miaka 20 na hivi sasa safari zimerejeshwa kwa wakazi na wasafiri wa maeneo hayo.

Mhe. Rais alizungumzia ukarabati wa reli za zamani kutoka Dar es Salaam hadi Isaka umbali wa kilometa 970 ambazo zimekua zikileta changamoto za hapa

>> Inaendelea Uk. 4

Na Mwandishi wetu TRC



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akiweka jiwe la msingi la Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kwa mara ya kwanza nchini katika hafla iliyofanyika eneo la Pugu jijini Dar es Salaam tarehe 12 Aprili 2017 .*

# RAIS MAGUFULI ALIPONGEZA SHIRIKA LA RELI TANZANIA, UJENZI WA RELI YA KISASA DAR ES SALAAM - MOROGORO MBIONI KUKAMILIKA

Inatoka Uk 3

na pale na kukwamisha safari kwa wananchi hasa ambao hupata unafuu mkubwa kwa kutumia usafiri wa reli.

“Huu ni uthibitisho kuwa kazi kubwa imefanyika katika sekta ya usafiri wa reli” aliongeza Rais Magufuli.

Hata hivyo Mhe. Magufuli alilieleza Bunge kuhusu kuboresha upatikanaji wa nishati ya umeme kwa kukamilisha miradi ya umeme ikiwemo mradi wa Kinyerezi 2 ambao umeongeza Megawat 240 na upanuzi wa mtambo wa  Kinyerezi 1 ambao utaongeza nguvu ya umeme kutoka Megawat 150 hadi 325 na pia alisema kuwa Serikali imeanza kutekeleza mradi mkubwa wa Bwawa la Nyerere katika bonde la mto Ruvu ambao utazalisha Megawat 2115.

“Gharama ya mradi huu wa Bwawa la Nyerere ni Trillion 6.5” alisema Rais Magufuli.

Miradi hiyo ya umeme ni kati ya vyanzo umeme vitakavyotumika katika uendeshaji wa treni ya kisasa ya SGR pindi itakapoanza ambapo chanzo kingine cha umeme kitakachotumika ni umeme kutoka Kidatu na Mtera hivyo mradi wa SGR utaendeshwa kwa umeme wa uhakika unaozalishwa ndani ya nchi kwa kutumia vyanzo vya ndani.

# MRADI WA UBORESHAJI WA RELI YA KATI – TIRP DAR ES SALAAM - ISAKA WAFIKA 85%, VIJANA ZAIDI YA 1000 WANUFAIKA

Na Mwandishi wetu TRC



*Muonekano wa sehemu ya kipande cha reli ikiwa imebadilishwa reli ya zamani yenye uzani wa ratili 60 na kuwekwa yenye uzani wa ratili 80 tayari wa ajili ya kuweka tabaka la juu la kokoto katika eneo la Mpiji mkoani Pwani hivi karibuni Juni 2020*

Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya Kati – TIRP unaogharimu Dola za Kimarekani Milioni 300 upo mbioni kukamilika baada ya mradi huo kufika 85% baada ya kazi kubwa iliyofanyika kati ya Dar es Salaam – Isaka umbali wa Kilometa 970 tangu ulipoanza rasmi utekelezaji wake mwezi Juni 2018.

Mradi umelenga kufanya ukarabati wa Reli iliyopo kwa kipande cha Dar es salaam - Isaka ili kuongeza uwezo wa kubeba mzigo toka chini ya Tani 13.5 za uzito wa ekseli hadi tani 18.5 kwa kutandika upya njia za Reli Kilometa 312, kukarabati njia ya reli Kilometa 658, kukarabati makaravati na madaraja zaidi ya 300, kuboresha mfumo wa mawasiliano, kukarabati vituo vya kupakia na kupakua mizigo vya bandari ya Dar es salaam, Ilala na Bandari kavu ya Isaka pamoja na kununua mitambo ya ukarabati wa njia, vichwa vitatu vya treni na Behewa mpya 44 za mizigo, na kukarabati vichwa viwili vya treni.

Mratibu wa mradi wa TIRP Mhandisi Mlemba Singo ameeleza kuwa kwa ujumla maendeleo ya kazi yamefikia 85% huku kazi kubwa inayoendelea kwa kipande cha Dar es Salaam – Kilosa ni kubadilisha Reli na Mataruma kwa kuondoa ya zamani na kuweka mapya pamoja na kuboresha tuta la reli ili viweze kuruhusu kubeba uzito na kwenda mwendokasi iliyopangwa.

Pia ameongeza kuwa kipande cha Dar es Salaam - Kilosa wako katika hatua za mwisho ambapo takribani Kilometa 50 kati ya Kilometa 289 ndizo zilizobaki katika kuboresha njia hiyo ya reli na kipande cha kutoka Kilosa hadi Isaka kazi zilizobaki ni chache zikiwemo uwekaji alama za reli, ujenzi wa mitaro na kuhakiki viwango vitakavyoiwezesha treni kwenda mwendokasi wa Kilometa 70 kwa saa.

"Kazi hii kwa ujumla itaisha mwezi wa Kumi mwaka huu lakini itaisha kwa vipande, kipande cha kutoka Dar es Salaam hadi Kilosa kazi itaisha mwezi wa kumi lakini kipande cha Kilosa – Isaka kazi itaisha mwezi wa saba" alisema Singo

Mhandisi Singo aliongeza kuwa "Tumeshanunua Behewa 44 za mizigo ziko tayari kwa ajili ya kazi hii, vichwa vinatengenezwa pamoja na kuboresha mfumo wa mawasiliano ambao utawezesha kufungwa Kompyuta katika Stesheni na kuongoza treni kwa kutumia Kompyuta"

Inaendelea Uk. 6

# MRADI WA UBORESHAJI WA RELI YA KATI – TIRP DAR ES SALAAM - ISAKA WAFIKA 85%, VIJANA ZAIDI YA 1000 WANUFAIKA

Na Mwandishi wetu TRC

Inatoka Uk. 3

Naye Msimamizi wa Mradi wa TIRP kipande cha Dar es Salaam – Kilosa Mhandisi Christopher Calist amesema kuwa kazi kubwa inayoendelea katika kipande hiko ni kubadilisha Mataruma ya reli urefu wa Kilometa 20 zilizobaki, huku kazi ya kubadilisha sehemu ambazo reli imezeeka kuanzia Pugu mpaka Soga urefu wa Kilometa 14 na ujenzi wa Madaraja ikiwa imekamilika

Aidha, kutokana na janga la ugonjwa wa Corona wahandisi wanaendelea na kazi katika maeneo ya ujenzi kwa kuzingatia tahadhari na maelekezo yanayotolewa na Wizara ya Afya nchini ili kuhakikisha afya za wafanyakazi zinakuwa kipaumbele.

Bi. Jesca Bakari ambaye ni Mtaalamu wa Afya anaeleza kuwa "Tunahakikisha wafanyakazi kabla hawajafika maeneo ya kazi tunawaandalia vifaa ambavyo vitawakinga na ugonjwa wa Corona, tuna sabuni, vitakasa mikono pamoja na maji, tunawapatia Barakoa na Glavu pia tunawapatia elimu juu ya kujikinga na Corona"

Halikadhalika, Mradi wa uboreshaji wa Reli ya Kati wawanufaisha vijana zaidi ya 1000 wanaofanya kazi katika mradi huo unaohusisha ukarabati wa reli kuanzia Dar es Salaa – Isaka.

Aidha, mbali na fursa za ajira na biashara zilizopatikana kupitia mradi huo wafanyakazi wanaoshiriki katika mradi wamepata fursa ya kuongeza ujuzi na utaalamu kuhusu teknolojia za kisasa zinazotumika katika ujenzi wa reli ambapo itakuwa chachu kwa taifa katika kuongeza ujuzi kwa wataalamu ambao wataendeleza ujuzi huo pindi wakandarasi watakapomaliza kazi nchini.

Msimamizi wa Mradi wa TIRP Ngerengere – Kilosa Mhandisi Felician Hechei ni amesema kuwa kazi kubwa inayoendelea katika eneo hilo ni utandikaji wa reli mpya yenye uzito wa ratili 80, urekebishaji wa mitaro makalavati na madaraja.

"Tuna takribani vijana 280 ambao wameajiriwa katika kipande hiki, kazi inaenza vizuri na kasi inazidi kuongezeka" alisema Mhandisi Hechei

Ally Ramadhani Amawe ambaye ni Msimamizi wa wafanyakazi katika Kundi la Mkata mkoani Morogoro anaeleza kuwa anapata kipato cha kuendesha familia yake kupitia kazi hiyo sambamba na kujitolea katika kulijenga taifa halikadhalika ameipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa jitihada za kutekeleza miradi ya kimkakati ambayo inawapatia fursa za ajira watanzania.

"Kiukweli wakati naanza kazi hii sikuwa na utaalamu wowote nilianza kama kibarua wa kawaida lakini sasa hivi nimepambana katika kuhakikisha majukumu ninayopewa nayafanyia kazi kwa usahihi mpaka nimekuwa kiongozi, serikali iko vizuri na Rais Magufuli yuko vizuri" alisema Ally Ramadhani

Naye Mashaka Hamis ameeleza namna ambavyo mradi huu umemuwezesha kuendesha familia yake pamoja na kufanya shughuli nyingine za kimaendeleo tangu ameanza kushiriki katika mradi huo, Hamisi amesema kuwa kupitia kazi hii ameweza kuongeza kipato na kununua kiwanja kwa ajili ya makazi "Katika Mradi huu nimefanya kazi kwa muda wa mwaka na miezi minne, mambo sio mabaya nimenunua uwanja na nina watoto watatu na wote wanaishi vizuri kwa kutegemea kazi hii" alisema Bwana Mashaka

Kukamilika kwa Mradi huu kutaboresha na kuongeza kiwango cha ubebaji mizigo kwa njia ya reli na madaraja, kuongezeka kwa mwendokasi wa treni toka Kilometa 30 hadi Kilometa 70 kwa Saa na hivyo kupunguza gharama za usafirishaji, kupunguza muda wa kupakia na kupakua mizigo kutoka Bandari ya Dar es salaam hadi bandari kavu ya Isaka kufikia hadi kufikia muda wa Saa 24.

Maendeleo haya ya mradi inaonesha dhahiri jinsi serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Mh.Rais Dk.John Pombe Magufuli ilivyodhamiria kuimarisha sekta ya miundombinu ya reli nchini na kuchochea Tanzania kuingia katika uchumi wa kati kwa haraka ifikapo mwaka 2025.

# WANANCHI WA KATA YA IHUMWA WAENDELEA KULIPWA FIDIA ILI KUPISHA UJENZI WA RELI YA KISASA



Na Mwandishi wetu TRC

Shirika la reli Tanzania - TRC laendelea na ulipaji wa fidia kwa wananchi 164 wa Kata ya Ihumwa jijini Dodoma hivi karibuni Juni 2020

Fidia hizo zinatolewa kwa wananchi mara baada ya TRC kutwaa rasilimali zao kwa lengo la kupisha ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kwa awamu ya Pili Morogoro – Makutupora, ambapo zoezi hilo ni endelevu kwa sasa linaendelea kufanyika Mkoani Dodoma katika kata ya Ihumwa.

Aidha, Kutokana na sera na sheria za ardhi ambayo inabainisha kuwa, fidia ni malipo yanayotolewa kwa mtu au taasisi kama mbadala wa mali yake kutokana na kuondolewa kwenye eneo lake lililotwaliwa kwa manufaa ya umma na kupangiwa matumizi mengine tofauti na yale yaliyopo kwa sasa.

Kwa hali hii inadhihirisha dhahiri Miradi inayosimamiwa na TRC imeletwa kwa lengo la kuleta faida kwa wananchi wa Tanzania hivyo serikali inawajibika kulipa fidia kupitia Shirika la Reli nchini.

TRC imetenga kiasi cha fedha za kitanzania 254,725,292/= ili kuwalipa fidia wananchi wa Kata ya Ihumwa na kuwataka punde tu wanapopokea hundi za malipo kupisha maeneo ndani ya siku 14 na mkandarasi kuendelea na ujenzi wa reli.

Katika hatua nyingine, maelfu ya wakazi wa Dodoma wanaendele kupokea stahiki zao za fidia ambazo kwa wengi imekuwa ni



*Afisa Uhasibu kutoka TRC Bwana Nassor Ramadhani akimsainisha Bwana Joseph Onera katika fomu ya kumbukumbu kabla ya kumkabidhi hundi ya Malipo ya fidia mkoani Dodoma Juni 2020*

fursa na njia ya kubadilisha na kuboresha maisha yao kutokana na kwamba fedha hizo zinapotolewa kwa wananchi kitengo cha mambo ya jamii kutoka Shirika la Reli pamoja na Viongozi wa ngazi ya kata mpaka Mkoa hutoa elimu juu ya matumizi bora ya fedha wanazolipwa hasa katika kuleta tija katika maendeleo ya familia, jamii na taifa kwa ujumla.

Hata hivyo, wananchi wametoa shukurani kwa Serikali na Shirika la Reli kwa kutimiza ahadi ya kulipa fidia ambayo kwa muda mrefu walikuwa wakisubiri, kwa upande mwingine wananchi wameonesha kufurahia mradi huo kwani umekuwa ni fursa kwa wakazi wa maeneo hayo ambapo vijana wa kike na wa kiume wamejipatia ajira mbalimbali huku wengine wakijikita katika fursa za biashara ndogo ndogo na ndoto kubwa ikiwa punde tu mradi utakapokamilika na kuanza kazi itakuwa ni fursa kwao na kwa maendeleo ya mji wa Dodoma hasa katika kukuza uchumi wa ngazi ya familia mpaka ngazi ya taifa.

## TRC YAREJESHA SAFARI ZA ABIRIA NA MIZIGO KATI YA DAR – MOSHI

Na Mwandishi wetu TRC

Shirika la reli Tanzania – TRC larejesha safari za treni za abiria na Mizigo kati ya Dar es salaam na Moshi mkoani Kilimanjaro ambao kwa kipindi cha takribani mwezi mmoja usafiri huu ulisitishwa.

Safari hizo zilisitishwa kutokana kuharibika kwa miundombinu ya reli kati ya eneo la Guiko na Hedaru urefu wa zaidi ya kilomita moja baada mvua maji kujaa katika bonde la mto Pangani kutokana na mvua kubwa zinazonyesha nchi jirani na kusababisha mafuriko kati ya mwezi Mei na Juni.

Shirika la reli Tanzania limejitahadi kurudisha njia na mpaka sasa ukarabati wa miundombinu katika eneo hilo umekamilika na treni za mizigo na abiria zimeanza kufanya kazi kama kawaida.

Mhandisi Shandrack Massawe amesema kuwa "Zaidi ya Behewa 170 za kifusi kimemwangwa katika kipande hiki cha Kilomita moja na nusu ambacho kimeathiriwa na mto Pangani kujaa maji'',, pia Mhandisi Masawe aliongeza kuwa kuna mizigo mingi ilikwama kuelekea Moshi hivyo walianza kupitisha na treni ya mizigo kutoka Tanga kwenda Moshi halafu baadaye treni za abiria itaanza safari zake kutoka Dar kwenda Moshi.

Shirika la Reli Tanzania lilijiwekea lengo la kurejesha njia hiyo ndani ya siku 14 lakini ndani ya siku 10 shirika lilifanikiwa kurudisha njia hiyo, hata hivyo shirika linatoa rai kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa reli kuacha shughuli za umwagiliaji kwani zinazidisha athari katika njia za reli.

## MRADI WA UBORESHAJI WA RELI YA KATI – TIRP ISAKA WAFIKA 85%, VIJANA ZAIDI YA 1000 WANU

wamepata fursa ya kuongeza ujuzi na utaalamu kuhusu teknolojia za kisasa zinazotumika katika ujenzi wa reli ambapo itakuwa chachu kwa taifa katika kuongeza ujuzi kwa wataalamu ambao wataendeleza ujuzi huo pindi wakandarasi watakapomaliza kazi nchini.

Msimamizi wa Mradi wa TIRP Ngerengere – Kilosa Mhandisi Felician Hechei ni amesema kuwa kazi kubwa inayoendelea katika eneo hilo ni utandikaji wa reli mpya yenye uzito wa ratili 80, urekebishaji wa mitaro makalavati na madaraja.

"Tuna takribani vijana 280 ambao wameajiriwa katika kipande hiki, kazi inaenza vizuri na kasi inazidi kuongezeka" alisema Mhandisi Hechei

Ally Ramadhani Amawe ambaye ni Msimamizi wa wafanyakazi katika Kundi la Mkata mkoani Morogoro anaeleza kuwa anapata kipato cha kuendesha familia yake kupitia kazi hiyo sambamba na kujitolea katika kulijenga taifa halikadhalika ameipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa jitihada za kutekeleza miradi ya kimkakati ambayo inawapatia fursa za ajira watanzania.

"Kiukweli wakati naanza kazi hii sikuwa na utaalamu wowote nilianza kama kibarua wa kawaida lakini sasa hivi nimepambana katika kuhakikisha majukumu ninayopewa nayafanyia kazi kwa usahihi mpaka nimekuwa kiongozi, serikali iko vizuri na Rais Magufuli yuko vizuri" alisema Ally Ramadhani

Naye Mashaka Hamis ameeleza namna ambavyo mradi huu umemuwezesha kuendesha familia yake pamoja na kufanya shughuli nyingine za kimaendeleo tangu ameanza kushiriki katika mradi huo, Hamisi amesema kuwa kupitia kazi hii ameweza kuongeza kipato na kununua kiwanja kwa ajili makazi "Katika Mradi huu nimefanya kazi kwa muda wa mwaka na miezi minne, mambo sio mabaya nimenunua uwanja na nina watoto watatu na wote wanaishi vizuri kwa kutegemea kazi hii" alisema Bwana Mashaka

Kukamilika kwa Mradi huu kutaboresha na kuongeza kiwango cha ubebaji mizigo kwa njia ya reli na madaraja, kuongezeka kwa mwendokasi wa treni toka Kilometa 30 hadi Kilometa 70 kwa Saa na hivyo kupunguza gharama za usafirishaji, kupunguza muda wa kupakia na kupakua mizigo kutoka Bandari ya Dar es salaam hadi bandari kavu ya Isaka kufikia hadi kufikia muda wa Saa 24.

Maendeleo haya ya mradi inaonesha dhahiri jinsi serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Mh.Rais Dk.John Pombe Magufuli ilivyodhamiria kuimarisha sekta ya miundombinu ya reli nchini na kuchochea Tanzania kuingia katika uchumi wa kati kwa haraka ifikapo mwaka 2025.

# ZIARA YA MHE. RAIS MAGUFULI KUKAGUA MRADI WA RELI YA KISASA MKOANI PWANI

Na Mpiga Picha wetu TRC




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa (wa pili kushoto) alipotembelea Stesheni ya Soga, hivi karibuni Juni 2020



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akizungumza na wananchi wa kijiji cha Soga (hawapo pichani) alipotembelea Stesheni ya SGR Soga mkoani Pwani, hivi karibuni Juni 2020



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akifurahia katika picha ya pamoja na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Isack Kamwelwe, viongozi wa mkoa wa Pwani na uongozi wa TRC katika stesheni ya SGR Soga mkoani Pwani, hivi karibuni Juni 2020



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akifurahia mandhari ndani ya treni ya uhandisi ya SGR wakati wa ziara ya kukagua mradi wa SGR mkoani Pwani, hivi karibuni Juni 2020



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kikongo (hawapo pichani) mara baada ya kushuka katika treni ya majaribio ya SGR, hivi karibuni Juni 2020


# UWEKAJI WA JIWE LA MSINGI LA UJENZI WA MAHANDAKI YA RELI YA KISASA MOROGORO



Na Mpiga Picha wetu TRC



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli (kati) akikata utepe kuashiria uzinduzi wa mitambo inayotumika katika uchorongaji wa Mahandaki ya reli ya kisasa Kilosa mkoani Morogoro hivi karibuni Juni 2020



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akiweka sahihi katika Handaki refu zaidi nchini ikiwa ni alama ya kumbukumbu mara baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Mahandaki Kilosa mkoani Morogoro hivi karibuni Juni 2020



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akipata maelezo kuhusu ujenzi wa Mahandaki kutoka kwa Mtaalamu wa ujenzi wa Mahandaki Mhandisi Amir Ahmed Kilosa mkoani Morogoro hivi karibuni Juni 2020.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akifurahi pamoja na baadhi ya viongozi alipokuwa akikagua Handaki refu la reli ya kisasa Kilosa Morogoro hivi karibuni Juni 2020



Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na baadhi ya viongozi wakitoka ndani ya Handaki refu la reli ya kisasa mara baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Mahandaki mkoani Morogoro hivi karibuni 2020.

# MRADI WA UBORESHAJI WA RELI YA KATI DAR - ISAKA MBIONI KUKAMILIKA




Mafundi wa Kampuni a CCECC inayo-karabati reli ya kati Dar es Salaam - Isaka wakiweka sawa sehemu ya reli ambayo ime-shabadilishwa katika eneo la Mkata Morogoro, hivi karibunii Juni 2020.



Mafundi wa Kampuni a CCECC wakiendelea na kazi ya kubadilisha reli kwa kuondoa reli ndogo yenye uzani wa ratili 60 na kuweka reli yenye uzani wa ratili 89 ili kuiongezea uwezo wa kubeba mzigo na kwenda kasi zaidi katika eneo la Mkata Morogoro, hivi karibuni Juni 2020.



Kazi ya kuondoa kokoto na kushindilia tuta ikiendelea kabla ya kuweka Mataruma na Reli mpya katika tuta la reli eneo la Mpiji mkoani Pwani, hivi karibuni Juni 2020.



Wafanyakazi wakiendelea na kazi ya kuweka Mataruma mapya juu ya tuta la reli eneo la Mpiji mkoani Pwani hivi karibuni Juni 2020



Wafanyakazi wakiendelea na kazi ya kuweka Reli mpya juu ya tuta la reli eneo la Mpiji mkoani Pwani hivi karibuni Juni 2020

# MCHANGO WA SHIRIKA LA RELI TANZANIA KATIKA KUIFIKISHA NCHI KATIKA UCHUMI WA KATI

Na Mwandishi wetu TRC

Shirika la Reli lipo katika maboresho makubwa ya kimkakati katika uendeshaji wa shughuli zake, ukizingatia Dunia hivi sasa iko katika ulimwengu wa Sayansi na Teknolojia hivyo Shirika limeanza kuboresha mifumo yake kwa kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa ukataji tiketi, mfumo wa Masijala, halikadhalika shirika linaandaa mfumo wezeshi ambao utawawezesha abiria kukata tiketi kwa kutumia simu ya kawaida ambayo si 'Smartphone', hakika haya ni mapinduzi ambayo yanakwenda sambamba na miradi ya uboreshaji na ujenzi wa miundombinu mipya ya reli ya kisasa bila kusahau mpango wa kukarabati Behewa za mizigo na abiria.

Gazeti la Reli na Matukio lilipata nafasi yakufanya mahojiano na wakuu wa Idara ambazo zinahusika zaidi na Uendeshaji kufahamu maboresho makubwa yanayofanyika katika huduma za usafiri wa reli nchini, mahojiano hayo yalikuwa kama ifuatavyo;

Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TRC Mhandisi Senzige kisenge ametoa ufafanuzi juu ya namna ambavyo mifumo ya ukataji tiketi inafanya kazi


**SWALI**
**Nini maana ya mfumo wa kieletroniki wa ukataji Tiketi (E – Ticketing)?**
**JIBU**

Ni mfumo unaotumika kusaidia katika mauzo ya Tiketi kwa wateja katika vituo vyetu vya treni pia kupitia 'Online', mfumo huu unamuwezesha mteja kununua tiketi bila kufika stesheni, akiwa na 'Internet Connection' tu ataweza kununua tiketi. Mfumo huu unawawezesha maafisa wa Shirika kuuza Tiketi kwa kutumia mfumo, awali Tiketi zilizokuwa zinauzwa ni za karatasi kwa kutumia vitabu lakini pia tumebadilisha mfumo na sasa maafisa wetu wanatumia mfumo mpya wa ukataji Tiketi, hii imewezesha kwa kiasi kikubwa kupunguza usumbufu kwa wateja, kuongeza makusanyo ya mapato yaani kupunguza mianya ya wizi kwa sababu kila tiketi inayouzwa tunaweza kujua imeuzwa na nani, muda gani na wapi kwa kiasi kikubwa imesaidia.

Mfumo huu pia umepunguza msongamano kwakuwa hakuna ulazima wa wateja kufika stesheni, anaweza kuhifadhi safari (Book) na akalipa kwa kutumia simu ya mkononi kwa sababu unavyofanya

Inaendelea Uk. 13

## HATUA 10 MUHIMU ZA KUKATA TIKETI



# MCHANGO WA SHIRIKA LA RELI TANZANIA KATIKA KUIFIKISHA NCHI KATIKA UCHUMI WA KATI



Inatoka Uk. 12

**JIBU:**
Mfumo umesaidia kwa kiasi kikubwa, kwa sababu ukilinganisha kipindi hiki ambacho tunatumia mfumo na kipindi ambacho hatukutumia mfumo kiukweli kwa sasa hivi mapato yameongezeka lakini pia umewezesha kuwa na usimamizi na udhibiti mzuri wa mapato na ufanisi umekuwa mkubwa zaidi.

**SWALI:**
**Mikakati gani mmepanga kuwasaidia wateja ambao hawawezi kutumia mfumo mpya wa ukataji tiketi?**

**JIBU:**
Bado tunaendelea kuwekeza katika mfumo kwa kuendelea kubuni na ufanisi utakuwa mkubwa zaidi na tunategemea hata watu ambao wanatumia simu za kawaida ambazo sio za kisasa nao wataweza kulipa na kupata tiketi. Pia tunaendelea kutoa matangazo kwa lengo la kuelimisha na kuwaelekeza wananchi namna ya kutumia mifumo yetu katikakukata tiketi.

**SWALI:**
**Mfumo wa ukataji tiketi kwa mtandao umeongeza vipi mapato?**

**JIBU:**
Mfumo wa ukataji tiketi umeongeza mapato kwa kiasi kikubwa na umesaidia ukilinganisha na kipindi ambacho hatukutumia mfumo na kwa upande wa watumishi hasa wale ambao wanahusika na wateja masuala ya ukataji tiketi umewarahisishia kazi kwa sababu mfumo unaunganisha mapato yote na muhasibu anapata taarifa za mapato ya sehemu zote tofauti na ilivyokuwa awali ambapo shirika lilikuwa linapoteza mapato.

Katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma, Behewa ni nyenzo kuu katika uafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya reli,hivyo Shirika limejipanga kuendana na kasi ya mabadiliko ya kimifumo katika kuhakikisha hakuna upungufu wa Behewa ili mifumo iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi, Mkurugenzi wa Uhandisi Mitambo Mhandisi Lameck Magandi ambaye anasimamiwa Vichwa vya treni na Behewa za abiria na Mizigo anafafanua kuhusu hatua iliyofikiwa katika ukarabati wa Behewa na mikakati iliyopo.

**SWALI:**
**Ukarabati wa Behewa umefika wapi mpaka sasa?**

**JIBU**
Ukarabati wa Behewa unaendelea vizuri, tulikuwa na ukarabati wa aina mbili ukarabati wa Behewa 40 uliopata fedha toka Shirika la Mpango wa Chakula Duniani - WFP ambazo mpaka sasa zimekamilika zimeshaanza kufanya kazi na mradi mwingine wa Behewa 200 ambao fedha za mradi jumla ya Shilingi Bilioni 4 zilitoka katika serikali ya Tanzania chini ya uongozi wa Rais Dkt.John Pombe Magufuli ambapo mpaka sasa kazi hiyo inaendelea na tumekarabati Behewa 96 kati ya 200 ambazo zipo tayari zinafanya kazi, Behewa zilizobaki zinasubiri vifaa kutoka nje na vifaa hivyo viko njiani na vingine vimeshaanza kuwasili tunatarajia kuendelea na kazi na kufikia mwezi Novemba mwishoni 2020 tutakuwa tumekamilisha Behewa zote 200.

**SWALI**
**Je, ukarabati wa Behewa ni endelevu au ni mradi wa muda mfupi?**



Inaendelea Uk. 14

# MCHANGO WA SHIRIKA LA RELI TANZANIA KATIKA KUIFIKISHA NCHI KATIKA UCHUMI WA KATI



Inatoka Uk. 13




JIBU

Zoezi la ukarabati wa Behewa ni endelevu, kwa sababu katika idadi tuliyokuwa nayo kama Shirika bado Behewa 600 zimesimama hazifanyi kazi kama Shirika tumeziwekea mkakati kuzifanyia ukarabati kwa kuanzia katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21 kuna fedha imetengwa kwa ajili ya kukarabati Behewa 200 kati ya 600, hili zoezi ni endelevu, wakati huo huo kuna fedha zimetengwa ya ukarabati Behewa 37 za abiria.

**SWALI**

**Behewa zikisharekebishwa zanaweza kufanya kazi kwa muda gani?**

JIBU

Behewa ambazo tunakarabati katika karakana zetu zitakuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa muda wa miaka 6 bila kuingia katika karakana kubwa isipokuwa ni matengenezo madogo madogo tu au endapo itapata ajali na huo ndio umadhubuti wa Behewa zetu tunazotengeneza katika karakana yetu ya Dar es Salaam.

Behewa tunazokarabati ni zile zilizofikisha muda wake wa kuingia karakana kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo makubwa (General Service Repair) hii hufanywa kila baada ya miaka 6 kwa hiyo Behewa hizi zilikuwa na hali mbaya na matokeo yake yakasimama yakawa hayafanyi kazi, tulichokifanya baada ya marekebisho haya zitaingia tena kwenye reli na kurudi tena kwenye matengenezo makubwa kama haya kwa muda wa miaka 6, hivyo watanzania wawe na imani na Shirika la reli Tanzania kwani kuna Behewa zitakuwa za kutosha kwa ajili ya watanzania.

Kwa hakika, pamoja na mambo mengine yanayofanyika katika Shirika ikiwemo ujenzi wa Reli ya Kisasa kuanzia Dar es Salaam hadi Makutupora Singida, uboreshaji wa Reli ya Kati Dar – Isaka, ufufuaji wa njia za rei ambazo ziliacha kufanya kazi pamoja na sera ya kuhamasisha uwekezaji hususani wa viwanda, mabadiliko haya tunayoyaona ndiyo msingi wa maendeleo ya Taifa la Tanzania yaliyoiwzesha nchi kufikia lengo la kufika uchumi wa kati ndani ya muda mfupi mapema mwaka 2020, ulinganisha maelngo iliyojiwekea ya kufikia uchumi huo mwaka 2025.

Watanzania wanastahili pongezi chini ya Uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania, katika suala hilila uchumi wa kati jukumu kubwa la Shirika la reli ni kuhakikisha kunakuwa na usafiri nafuu, wa uhakika na wa haraka kwa njia ya reli na hakika Shirika limeweza na limeonesha uthubutu katika kusimamia miradi yake ili iweze kusaidia atanzania na nchi kwa ujumla kuendelea kupaa kicuhumi siku zijazo.



SHIRIKA LA RELI TANZANIA
Mtaa wa Reli/Barabara ya Sokoine
S.L.P 76959
Dar es Salaam
TANZANIA
Barua pepe; info@trc.co.tz
Tovuti; trc.co.tz
Simu ya Bure; 0800 110 042

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
SHIRIKA LA RELI TANZANIA

| | |
|---|---|
| MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk |
| MHARIRI MSAIDIZI | Sami Omary |
| MTAYARISHAJI | Sami Omary |
| MAKALA | Aziza Charles |
| HABARI | Tracylinda Nganga |
| PICHA | Seleman Kadiko |
| KIBONZO | Hassan Said |

tzrailways TRC Reli TV

Reli Yetu | Maendeleo Yetu | Taifa Letu #TRCMpya